



Ni Vipi Utaonekana



Tukirudi nyuma mwaka 1999 galaxi hii ilikuwa inaelea kwa utulivu na hakuna aliyekuwa anajali hapa Duniani. Ghafila utulivu huo uliondolewa na mlipuko wa kupendeza. Ilikuwa in kifo cha nyota iliyokuwa kubwa, ambao ni moja kati ya matukio yenye nguvu sana ya asili. Tunaita mlipuko hii Supanova, ambapo mlipuko huu ulitoa mwanga mwingi wa kupita hata ule wa galaxi nzima pamoja na wenyewe.

Muonekano huu wa kushangaza wa galaxi iliyopo karibu nasi ulinaswa na wanaastronomia waliokuwa wanasoma madhara baada ya mlipuko. Waliona mng'ao wa supanova unafifia kadri miaka inavyozidi kwenda. Ulififia kiasi kuwa ile supanova iliyokuwa inaonekana kwa urahisi, ilikuwa haonekani tena kwa urahisi kwenye hii picha. Ijapokuwa supanova hii imefifia sana wanaastronomia waliweza kupata taarifa chache kuhusiana na nyota iliyolipuka. Ambayo ilikuwa kubwa sana kabla ya kifo chake – ukubwa wa zaidi ya mara nane ya Jua!

Picha hii inaweze isionyesha mwanga unaong'aa wa supanova, lakini inaonyesha baadhi ya taarifa muhimu. Galaxi hii inajulikana kama 'spiral galaxi' kama ilivyo kwa Milky Way. Zimepewa jina hilo kwa sababu ya mbo lake linalofanana na kisahani chenye mikoni mirefu iliyoshikizwa katika kiini cha galaxi hii. Mikono ya galaxi katika picha imekolezwa na sehemu za rangi ya blue zenye nyota changa, gesi zinazowaka na magimba yenye giza.

COOL FACT

Supanova moja inaweza kutengeneza nishati nyingi kuliko ile inayoweza kutengenezwa na Jua katika maisha yake yote. Na Jua letu litaishi miaka inayokaribia bilioni 10!

